Kujifunza Kufanyakazi Na Watoto Waishio Katika Mazingira Hatarishi Zaidi Na Familia Zao.

Mradi wa Ushirikiano wa Ustawi wa Jamii kuhusu VVU/UKIMWI kwa ajiri ya Watoto Yatima na waishio katika mazingira Hatarishi zaidi nchini Tanzania

Siku ya 6

Msaada na Mabadiliko ya Tabia kwa watoto waishio katika mazingira hatarishi zaidi na familia zao.

Mchakato Wa Huduma Za Ustawi Wa Jamii Kwa Watoto Yatima Na Watoto Waishio Katika Mazingira Hatarishi Walioathiriwa Na VVU/UKIMWI

1. Kuwafikia na kuwatambua
2. Kujenga uhusiano na watoto yatima na familia zao
3. Kutathmini mahitaji na uwezo wao
4. Kutengeneza mpango wa huduma: ambao ni pamoja na mitandao, utambuzi na kutoa rufaa kwenye vyanzo vingine vya huduma.

Mchakato Wa Huduma Za Ustawi Wa JamiiKkwa Watoto Yatima Na Watoto Waishio Katika Mazingira Hatarishi Na Walioathiriwa Na VVU/UKIMWI

5. Utekelezaji wa mpango wa huduma.
- Tambua na toa rufaa kwa ajili ya rasilimali nyinginezo
- Kutoa huduma za moja kwa moja Kutatua matatizo, kusaidia na kuratibu
- Kuwawezesha na kuwasaidia walezi.
- Shughulikia masuala ya kinga na huduma dhidi ya VVU.

6. Upimaji wa maendeleo, kurejea mpango wa huduma na ufuatiliaji kwa kupitia kesi menejimenti kunakoendelea, Msaada wa familia na utetezi

Malengo

Kufikia mwisho wa siku , Msaidizi Ustawi wa Jamii wataweza:

- Kuelezea misingi ya kubadili tabia na hatua za modeli ya kubadili tabia.
- Kuelezea dhana ya kupunguza hatari na jinsi ya kusaidia maamuzi ya kupunguza hatari.
  - Zinazotokana na tabia hatarishi kama vile utegemezi na visababishi vya VVU.
- Kuonyesha stadi za kutatua matatizo Kwa kutumia mfumo wa familia na kupunguza hatari kwa watoto waishio katika mazingira hatarishi, familia na walezi.
- Kuelezea mchakato wa maombolezo na kupotelewa katika mazingira ya watoto waishio katika mazingira hatarishi na familia zao.

Mpango Wa Mabadiliko Ya Tabia

Msaidizi Ustawi wa Jamii kama chachu ya mabadiliko katika Kuwasaidia watoto waishio katika mazingira hatarishi na familia zao.

Mpango Wa Mabadiliko Ya Tabia

Mpango wa Mabadiliko ya Tabia una mambo matatu:

- Mabadiliko kulingana na mazingira.
- Mabadiliko mapya kutokana na hamasa ya ndani ya mtu.
- Mabadiliko yanayolenga kiasi fulani cha tabia husika kutokana na mazingira mbalimbali.

Mpango Wa Mabadiliko

- Watu hubadilika ili kukabiliana na hali(mazingira) ili kukidhi mahitaji na kutimiza malengo yao.
- Mchakato hai, wenye nguvu ambao watu wanawanashrikiana na mazingira yao kama mfumo wa kiikolojia ambapo kila mmoja husaidia kumbadili mwingine.
- Watu wanaweza kubadili mazingira yao ili kuendana na mahitaji yao ya kimwili na kisaikolojia.

Mabadiliko Huathiriwa Na…

- Maendeleo ya makuzi, kupevuka
- Mabadiliko kulingana na hali:
- Kupotelewa katika familia,
- Kukosa kipato
- Nguvu nyingine zilizo nje ya mtu mwenyewe zinazomfanya awe na tabia za namna fulani
- Kubadilika kwa majukumu ya kifamilia
- Uamuzi wa mtu binafsi kubadili tabia anayoiona kuwa na madhara na/au haikubaliki
- ***mfano***: Tabia ya kufanya Ngono isiyo salama inaweza kupelekea matatizo ya kiafya.
- ***mfano:*** Taratibu za kimila (m.f. Ukeketaji wanawake) umetambulika kuwa si salama katika jamii.

Mabadiliko Yanaathiriwa Na

- Sababu nyinginezo (kwa mtu mwenyewe au hali)
- Shinikizo rika
- Kuongezeka ufahamu kuhusu matokeo ya tabia zenye madhara.
- Shinikizo kutoka kwa Famii au jamii (chanya au hasi)
- Dalili za magonjwa na/au kuchoka kwa mwili
- Shinikizo chanya au hasi la kijamii toka katika ngazi zote za kijamii.
- Shinikizo linalohusiana na sera.

Kupunguza Vihatarishi

- Kupunguza vihatarishi ni modeli ya kubadili tabia inayoweza kuwa ya msaada unaoweza kusaidia katika kuelewa jinsi ya kubadili tabia na jinsi msaidizi ustawi wa jamii anavyoweza kusaidia katika mchakato. Kunazingatia kushughulikia vihatarishi badala ya vitendo /tabia.
- Mikakati ya kupunguza vihatarishi hupunguza madhara wakati unampa mteja nafasi, muda na mrejesho chanya unaohitajika kubadili tabia ya kudumu.
- Kupunguza Vihatarishi kunaweza kutoa njia inayofaa kubadilika baada ya muda kwa kupunguza tabia hasi au kuimarisha tabia chanya.

Ni Ipi Mifano Mingine Ya Kupunguza Tabia Hatarishi (Hasi Au Chanya)

Bungua Bongo

Ni Ipi Mifano Mingine Ya Kupunguza Tabia Hatarishi (Hasi Au Chanya)

- Kupunguza idadi ya wapenzi
- Kuongeza matumizi ya kondom
- Kupunguza kiasi cha matumizi mabaya ya madawa.

Jukumu La Msaidizi Ustawi Wa Jamii Katika Mpango Wa Mabadiliko Ya Tabia

- ***Mpango wa kubadili Tabia*:** ni utaratibu wa kutatua matatizo unaotegemea:
- Tathimini ya tatizo
- Ufahamu wa mtu binafsi kuhusu utayari wa kubadilika
- Afua zinalenga kuleta mabadiliko.
- Msaidizi ustawi wa jamii anafanya kazi kama chachu ya mabadiliko pamoja na mtoto/familia na kupanga mipango wote pamoja nao kwa ajili ya mabadliko.
- ***Mabadiliko yenye mpangilio yana kusudi maalumu*** na yanaongeza uwezekano wa kupata matokeo yanayoweza kutabiriwa kutokana na juhudi za kuleta mabadliko. (Hefferman, et al., 1988:10)

Kupunguza Vihatarishi Na Kubadili Tabia

- ***Kupunguza vihatarishi au kupunguza madhara ni utaratibu wenye mwelekeo kwamba:***
- Kubadili Tabia ni mchakato unaotokea kwa muda kuliko kuwa ni tukio la mara moja.
- Kupunguza Vihatarishi kunajumuisha mambo mengi, ikiwemo mahusiano ya kisaikolojia pamoja na mazingira.
- Mikakati ya kupunguza vihatarishi ni lazima ipangiliwe katika hatua ndogondogo ili iweze kutekelezwa kwa ufanisi.

Hatua Za Mabadiliko

Mzunguko Wa Mabadiliko

- Modeli ya"Mzunguko wa mabadiliko" unaelezea ngazi(hatua) za mabadiliko ambazo kila mtu hupitia katika safari ya kuelekea kubadili tabia.
- Modeli hii ya" Hatua ya mabadiliko"ilibuniwa na Prochaska pamoja na Diclementi (1982) ambao walitofautisha hatua sita katika mchakato wa kubadili tabia.

Mzunguko Wa Mabadiliko

- Modeli hii haiwasilishwi ili kupendekeza kuwa mabadiliko ni kitu chepesi au rahisi, ila kwa ajili ya kusisitiza kuwa mabadiliko ni jambo lenye mchanganyiko wa mambo na yanahusisha mchakato ili yaweze kutokea.
- Msaidizi ustawi wa jamii anaweza kupima pale ambapo mtu yuko kwenye mchakato wa mabadiliko na kuchagua utaratibu wa jinsi ya kushughulikia kwa usahihi kulingana na hatua ya ngazi husika.
- Hii humsaidia msaidizi ustawi wa jamii " kuanzia pale mteja alipo"

Hatua Za Mabadiliko

1. ***Hakuna mipango ya mabadiliko:*** (Hakuna fikra za mabadiliko)
2. ***Kufikiria*** kuhusu kubadilika(fikra za mabadiliko)
3. ***Uamuzi wa*** kubadilika (Uamuzi)
4. ***kubadilika***Tabia(Kitendo)
5. ***Kuendeleza*** mabadiliko(kudumu katika mabadiliko)
6. ***Kurudia Nyuma: Kurudia kwenye tabia yenye athari*** (kurudia)

Mzunguko Wa Mabadiliko

Hatua Ya Kutobadilika

- Mtu hana wazo lolote kuhusu kubadilika, au hafahamu kuwa anatatizo au anapuuzia, au yuko katika hatua ya kukana tatizo**.**
- Jukumu la msaidizi ustawi wa jamii
- Toa taarifa na mrejesho kujenga uelewa kuhusu tatizo na uwezekano wa kufanya mabadiliko.
- Taarifa isihukumu.
- Husisha familia, mamlaka za kijamii na jamii kwa ujumla ili kusaidia kuliwasilisha wazo la kubadili tabia
- Mhakikishie kuwa msaada chanya kwa ajili ya mabadiliko utakuwepo.

Hatua Ya Kufikiria Kufanya Mabadiliko

- Kufikiria kuhusu mabadiliko, kwa namna moja au nyingine anaona kuwa anawajibika kwa tabia aliyo nayo,lakini bado hajafanya maamuzi ya dhati kufanya mabadiliko.
- Yaweza kuwa na mchakato mrefu unaohitaji mtu kusogea kuanzia kwenye kukubali tatizo, kukubali baadhi ya majukumu mpaka kuwa na hisia za haja ya kufanya kitu kuhusu tatizo.
- Anafikiria mabadiliko lakini pia analiogopa hilo wazo hivyo anaweza kulikataa.
- ***Jukumu la msaidizi ustawi wa jamii:***
- Msaidie mlengwa kuweka uwiano kwa kupendelea zaidi mabadiliko, zaidi ya kitu kingine.
- Msaidie mlengwa aone faida za kubadilika na athari za kutobadillika.

Hatua Ya Kufanya Maamuzi

- Kuamua kufanya kitu kuhusu tatizo . Kufanya uamuzi wa kufanya mabadiliko lakini bado hujaweza kuweka maamuzi hayo kwa vitendo.
- ***Jukumu la msaidizi ustawi wa jamii.***
- Msaidie mlengwa kuwa na mkakati wa mabadiliko ambao unazingatia:
- Muda
- Una ukweli
- Unaweza kuufikia
- Unakubalika
- Unawezekana
- Ni sahihi
- Unaufanisi.

Hatua Ya Kubadilika

Kuchukua hatua ya kufanya mabadiliko

- ***Jukumu la msaidizi ustawi wa jamii:***
  - Toa msaada endelevu
  - Fanya utetezi kwa familia na jamii ili kuepuka lawama na kusaidia mabadiliko.
  - Saidia kukamilisha hatua za mabadiliko.

Hatua Ya Kuendeleza Mabadiliko

Kuendeleza au kudumisha tabia mpya.
Jukumu la msaidizi ustawi wa jamii.

- Msaidie mtu kuendelea katika tabia mpya
- Toa vitendea kazi kama vile: vitu au ujumbe wa kukumbushia, kalenda, vijizawadi vidogovidogo ili kuendeleza tabia chanya
- Tambua uwezekano wa kurudia tabia ya mwanzoni(kurudia)
- Msaidie mtu atambue na kutumia mikakati ya kuzuia kurudia tabia ya mwanzoni
- ***Msaidie mlengwa kutambua kuwepo kwa mafanikio ya badiliko la tabia kunakoendelea.***

Hatua Ya Kurudia Tabia

Kurudi nyuma kwenye tabia ya awali:

- Kunaweza kupelekea uamuzi mpya kuendelea kufanyia kazi tatizo.
- Kurudia tabia hatimae kunaweza kupelekea kurudia tabia ya awali ambayo itamweka mtu kurudia katika hatua ya mwanzo kabisa ya mduara wa mabadiliko.

Kusaidia Familia Kutatua Matatizo

Katika kuzisaidia familia kutatua matatizo, Msaidizi ustawi wa jamii mara zote anafanya kazi kama:

- Msaidizi
- Kiunganishi cha huduma katika jamii(kama ilivyo jadiliwa siku ya 5)
- wakala wa utetezi katika familia na jamii.

Hatua Ya Kurudia Tabia

- ***Jukumu la msaidizi ustawi wa jamii***
- Mhakikishie mtoto/familia kuwa bado mabadiliko yanawezekana na kuwa kurudia tabia ni kitu cha kawaida.
- Mhakikishie mtoto/mwanafamilia kuwa msaada wetu utaendelea hata kama tabia itabadilika
- Epuka kulaumu, kuhukumu na mwitikio mwingine wowote ulio hasi.
- Mhakikishie mtoto/familia kuwa mabadiliko chanya yanaweza kudumu,
- Tambua hali iliyopelekea kujirudia kwa tabia.
- Msaidie mtoto/familia kuelewa jinsi ya kubadilika na masharti ya kufanya badiliko la tabia chanya iendelee

Jukumu La Msaidizi Ustawi Wa Jamii:

Kutatua Matatizo Kwa Ajili Ya Kubadili Tabia Na Kupunguza Vihatarishi.

Nani Ni Rasilimali Ya Jamii? Nani Anayeweza Kusaidia Kutatua Matatizo?

- Msimamizi wa wasaidizi ustawi wa janii.
- Madaktari wa afya, wauguzi, waalimu.
- Wanasihi wenye uzoefu katika jamii
- Viongozi wa dini
- Wanasihi wenye uzoefu wa hali mbali mbali.
- Wanasihi wazoefu wa shule.
- Wataalamu wa afya ya akili au wa watumia madawa wenye uzoefu
- Maafisa ustawi wa jamii.

Msaidizi Ustawi Wa Jamii Kama Wakala Wa Kutatua Matatizo

- Kusaidia familia kupata mahitaji yao ya msingi (chakula, mavazi, malazi)
- Msaidie mlezi au mtoto kukubali msaada kwa ajili ya kutatua matatizo
- Wasaidie wana familia wengine kutoa msaada wa shughuli za kutatua matatizo.
- Panga mpango wa kuwaunganisha na huduma mtoto,familia na vyanzo vya rufaa ikiwa kuna umuhimu. (tulijadili siku ya 5)
- Ratibu pamoja na watoa huduma wengine ili kuunganishwa huku kwa huduma kuwe na ufanisi na kwa wakati muafaka.

Jukumu La Msaidizi Ustawi Wa Jamii: Kutatua Matatizo Ili Kuleta Mabadiliko

Msisitizo upo katika mchakato wa mabadiliko, ambao unahitaji

- Kujenga na kuendeleza uhusiano mzuri na mtoto/familia katika mazingira ya mabadiliko.
- Tambua na chunguza jinsi ya kuwezesha mabadiliko.
- Tambua na chunguza utashi wa kubadilika na vikwazo vya mabadiliko.
- Chunguza msaada unaohitajika kwa mabadiliko ya muda mrefu
- Fanya uchaguzi wa utatuzi na tengeneza mpango wa kubadili tabia.

Maelezo Ya Ujumla: Modeli Ya Kutatua Matatizo

1. Kujenga mahusiano
2. Uchunguzi wa Tatizo
3. Kulielewa Tatizo
4. Mpango wa Utekelezaji na tathmini ya matokeo.

Modeli Ya Kutatua Matatizo

1. Kujenga mahusiano mazuri na mawasiliano, kunahitaji stadi za mawasiliano yasiyohukumu.

- Namna ya sauti
- Tabia ya kuhudumia
- Uulizaji maswali
- Kurudia kilichosemwa pasipo kupoteza maana
- Kurejea hisia
- Kutoa muhtasari
- Kuto kuhukumu

Rejea mada za awali—toa mjumuisho na urejee mada ya kujenga mahusiano ma familia pamoja na mtoto.

Modeli Ya Kutatua Matatizo

2. Uchunguzi wa Tatizo: Fanya tatizo liwe mahususi.

- Je Tatizo ni nini?
- Je Lilianza lini?
- Je ni tatizo kwa kiasi gani?

Modeli Ya Kutatua Matatizo

3. Kulielewa Tatizo

- Weka alama ya hisia– kuomboleza, kufurahi, kukasirika
- Baini lugha ya alama , ujumbe/Hisia na zirudie tena.
- Kubali na thibitisha kuwepo kwa ukinzani au hisia za migongano
- Unganisha hisia kwenye ukweli au kwenye tatizo.

Modeli Ya Kutatua Matatizo

4. Kupanga Mpango wa utekelezaji na tathmini ya matokeo.

Ni zipi shughuli zinzowezekana?

Bungua bongo

Modeli Ya Kutatua Matatizo

4. Kupanga mpango wa utekelezaji na kutathmini matokeo.

- Panga pamoja na mtoto au mlezi
- Chunguza jaribio lililotangulia la kutatua tatizo.
- Chunguza jinsi ya kutatua tatizo kwa sasa.
- Washirikishe mawazo yako kuhusu njia za utatuzi zinazowezekana.
- Fuatilia mpango wa utekelezaji.

Modeli Ya Kutatua Matatizo Unasihi

Chagua njia mojawapo ya utatuzi na tengeneza mpango.

- Msaidie mtoto au mwanafamilia kuchagua suluhisho lenye uhalisia
- Utatuzi upi utafanya kazi vizuri? Kwanini?
- Ni mkakati gani unaowezekana kwa mtoto au familia?
- Kwa jinsi gani na lini mtu ataweza kutatua tatizo alilonalo (Mpango mahususi)?

Jukumu La Msaidizi Ustawi Wa Jamii: Ufuatiliaji Wa Mpango

- Saidia kuanzishshwa kwa mtandao wa kusaidia kutatua matatizo ya familia na jamii.
- Amua nani atafanya nini, lini, na wapi.
- Toa rufaa kwa usahihi.
- Fuatilia kuona kama mpango ulizingatiwa.

Maisha ya mtoto III: Kuomboleza na kupotelewa

Maelezo Ya Ujumla: Kuomboleza Na Kupotelewa

- Watoto wote wanakabiliwa na kuomboleza na kupotelewa wanapotenganishwa na wazazi/mzazi kwa sababu ya ugonjwa, kifo au kutelekezwa.
- Kama ilivyo katika maeneo mengine ya maendeleo ya binadamu, kuomboleza na kupotelewa kunategemea miongoni mwa baadhi ya sababu za kijinsia na hatua za makuzi.

Maelezo Ya Ujumla:Kuomboleza Na Kupotelewa Kwa Watoto

- Hisia kuhusu kuomboleza na kupotelewa zinaweza kusababisha tabia nyingi tofauti zinazoashiria kuomboleza na kupotelewa, kwa mfano:
- Hasira.
- Kuhuzunika.
- Kufanya shughuli zaidi kuliko kawaida
- kujitenga
- Hisia hizi ni sahihi lakini zinaweza kusababisha tabia ambazo zina madhara kwa mtoto, watu wengine au mali.

Mchakato wa kuomboleza

- ***Hisia kuhusu kuomboleza na kupotelewa zinaweza kusababisha tabia nyingi zinazoashiria kuomboleza au kupotelewa. Kwa mfano:***
- Hasira
- Kuhuzunika
- Kufanya shughuli zaidi kuliko kawaida
- kujitenga

Mchakato Wa Kuomboleza

- kuomboleza, kama ilivyo kubadili tabia,ni mchakato ambao uko katika sura ya mzunguko. Watu wanao kabiliwa na kuomboleza na kupotelewa wanaweza kurudia hatua za mwanzo kutegemeana na mazingira. Tukio lisilo na uwiano au mshtuko wa maono linaweza kuibua hisia za kuomboleza kwa upya zilizo sababishwa na kupotelewa zamani.
- Je unafikiri zipi ni hatua katika mchakato wa kuomboleza?

Bungua Bongo

Hatua Za Kuomboleza

- Mshtuko/Ukanaji
- Hasira
- Jadiliana
- kuhuzunika na Sonona
- Kukubali

Angalizo:

- Kila mtu anaweza kukuombolezaka kwa namna ya tofauti.
- Inawezekana kuto pitia hatua kwa mtiririko na inaweza kwenda nyuma na mbele kwenye hatua..

Kuomboleza Kunakoendelea

- Tunaweza kukuombolezaka hata baada ya kuamini kuwa tumefikia kukubali hali.
- Watoto hurejea kuomboleza katika kila hatua ya makuzi.
- Watoto wanaweza kuonekana kuwa wamesahau kuhusu kupotelewa kwa muda, lakini ghafla huweza kuonekana mwenye huzui sana na mwenye hasira..
- Mara nyingine watoto wanaonekana kama wamefikia kukubali lakini wametunza tu matatizo, hisia zao. Hisia hizi zenye nguvu zinaweza kujitokeza katika siku za baadae.
- Kupotelewa mara nyingi kunachochea hisia za nguvu, Lakini hisia zisizo na ufumbuzi kutokana na kupotelewa zamani

Madhara Ya Kuomboleza Kunakoendelea

- Watoto waliotenganishwa na wazazi wao kwa sababu ya ugonjwa, kifo au sababu nyinginezo watakuwa wakikuombolezaka.
- Maumivu ya kutenganishwa na kupotelewa ni aina ya mshituko wa maono.
- Watoto wanaweza kukwama katika ngazi moja, au hata kurudi nyuma kwenye hatua ya mwanzo ya maendeleo.

Matokeo Ya Kuomboleza Kunakoendelea

- Watoto waliotenganishwa na wazazi wanaweza kuwa na hasira, sonona, au wakatili.
- Tunapomwona mtoto ambae anahasira hii inaweza kuashiria kupotelewa na maumivu aliyopitia (“mara zote unapoona hasira, jaribu kutafuta maumivu aliyonayo”)
- Watoto wengine wanaweza kuonekana wachangamfu na wasiojali. Hii ni njia mojawapo ya kuficha maumivu ya kupotelewa.

Matukio Na Mazingira Yanayo Chochea Kuomboleza

- Kumbukumbu za matukio muhimu
- Kumbukumbu za kuzaliwa
- Harusi
- Likizo
- Nyimbo maalumu, vyakula, n.k.
- Sehemu zenye uhusiano na kupotelewa.
- Watu wenye majina yanayofanana na au kufanana na mtu aliyepotea.

Sababu Zinazoathiri Uwezo Wa Kuomboleza

- Asili ya kupotelewa
- Afya na uwezo wa kujiamini
- Umri wa wakati wa kila kupotelewa
- Watoto ambao hawaelewi dhana ya kifo wanaweza kushindwa kuomboleza kwa usahihi hali inayopelekea kuchelewa kuomboleza.
- Kiwango cha ukaribu kwa mtu aliyepotea.
- Hatari ya ndani anayoipitia mtu binafsi kuhusu kupotelewa.

Sababu Zinazoathiri Uwezo Wa Kuomboleza

- Mazingira yanayosababisha kupotelewa.
- Je kuna tofauti ya kuomboleza kati ya kupotelewa kwa ghafla na kupotelewa kulikochukuwa muda mrefu?
- Idadi ya kutengana kwa kulikotangulia hapo awali
- Msaada unaotolewa wakati wa mchakato wa kupotelewa (kabla,wakati wa au baadae)
- Msaada uliotolewa wakati wa, na baada ya kupotelewa.

Changamoto Za Kusaidia Kwa Msaidizi Ustawi Wa Jamii

- ***Kumsaidia mtoto aliyepotelewa kunaweza kuwa na changamoto kwasababu:***
- Kutenganishwa na kupotelewa ni hali yenye maumivu sana.
- kuomboleza kunakoendelea kunaweza kukatisha tamaa.
- Hakuna raha ya kuwa na watoto ambao wamekasirika na masikitiko.
- kuomboleza kwa watu wengine hutukumbusha maumivu tuliyonayo wenyewe.
- Kufanyakazi na watoto au familia iliyopotelewa kunahitaji uvumilivu. Kushughulika na kupotelewa kwenye maumivu kunachukuwa muda mrefu zaidi hata kwa maisha yote.

Jinsi Gani Ya Kumsaidia Mtoto

- Hamisha mtazamo wa mtoto toka kwenye kujihisi kutokuwa na thamani mpaka kwenye kujisikia ana uwezo na matumaini.
- ***Toa taarifa:***
- Watoto wanahitaji taarifa kuhusu wao wenyewe, familia zao, hali zao,maamuzi yanayofanyika kususu wao.
- Kuwa na taarifa kuhusu maisha yao huwasaidia watoto kujisikia wana ulinzi na wako salama.

Jinsi Gani Ya Kumsaidia Mtoto…

- Kuhakikisha kuwa watoto wameunganishwa kuhusu mahusiano binafsi pamoja na mazingira kwa upana wake.
- punguza pengo la upotevu alilonalo mtoto kwa kuendeleza mahusiano aliyonayo mtoto na ndugu zake, wanafamilia wengine, watu wengine ambao ni wa muhimu kwa mtoto.
- Fanyia kazi suala la kuwa na mahusiano yenye ukaribu na watoa huduma.
- Tafuta misaada ya kifedha kwa ajili ya mtoto.

Jinsi Gani Ya Kumsaidia Mtoto…

- Uwanachama wa kikundi
  - Mhusishe mtoto katika kikundi kinacholingana na umri wake : Vikundi vya kifamilia vyenye mtazamo kwenye mambo yenye manufaa kwa mtoto. n.k.
- Majukumu yenye maana
  - Msaidie mtoto ili aweze kufanya majukumu yenye maana katika familia, shuleni, katika vikundi vya wanarika. n.k.

Jinsi Gani Ya Kumsaidia Mtoto…

- Saidia kutambua uwezo ambao ni chanzo cha kumpa furaha.
- Furahia mafanikio ya mtoto.
- Mjumuishe mtoto kwenye familia, shughuli za kimila pamoja na sherehe.
- Fundisha maadili na mitazamo inayojenga:
- Mhusishe mtoto katika maswala ya kiimani za dini au shughuli nyinginezo zinazo fundisha maadili na tabia njema ili kuongoza tabia za mtoto.
- Mara zote onyesha mfano wa maadili na tabia njema unazopenda mtoto awe nazo.

Jinsi Gani Ya Kumsaidia Mtoto…

Historia ya mtu binafsi

- Kutokana na umri wao mdogo, watoto yatima na wale waishio katika mazingira hatarishi mara nyingi husahau taarifa za matukio muhimu katika maisha yao. Wanaweza kujenga hisia zenye mchanganyiko kuhusu historia zao wenyewe.
- Hifadhi taarifa kwa ajili ya mtoto zinazohusu matukio ya maisha yao binafsi kama vile: Walizaliwa wapi, sehemu walizowahi kuishi, watu waliwahi kuishi nao, shule walizosoma, watu ambao wamekuwa na umuhimu kwa maisha yao. Vitabu vya kumbukumbu au vitabu vinginevyo au masanduku yanaweza kusaidia katika hili.

Jinsi Gani Ya Kumsaidia Mtoto…

- Hakikisha kuwa mtoto ameunganishwa sehemu.
- Watu wengi wana mahusiano ya kihisia za ukaribu kwa sehemu wanayoitambua kuwa “nyumbani “ Watoto ambao wamehamahama mara nyingi au kuishi mitaani wanaweza wasiwe na hisia za wapi ni nyumbani.
- Imarisha hali ya maisha ya mtoto, punguza kuhamahama ili kumsaidia mtoto ili kujenga hali ya uimara na kujiona ni sehemu ya.

Jinsi Ya Kuwasadia Walezi

- Msaidizi ustawi wa jamii anaweza kuwa na matokeo mazuri zaidi kwa mtoto kwa kuwajengea uwezo wazazi na walezi kuwa na malezi na muundo sahihi.

Wasidie walezi kuelewa kuwa:

- Jinsi mtoto anavyokuwa na kuendelea, Hatua zote za kuomboleza zinaweza kujitokeza tena na tena.
- Mtoto mwenye kuomboleza anaweza kuchanganyikiwa kuhusu mahusiano ya mzazi na mtoto.

Jinsi Ya Kuwasadia Walezi

- Msaidie mtoto kuwa na uvumilivu katika kujenga stadi.
- Kumsaidia mtoto kunahitaji msaada unaoendelea kwa kipindi cha muda fulani.
- Mahitaji ya mtoto na hisia ni muhimu.
- Mtoto yuko salama na atapata matunzo.
- Mahitaji ya mtoto yanaweza kuelezewa na kufikiwa.
- Wazazi wanaweza kuwa na utaratibu endelevu wa kuaminika.

Muhtasari

Bungua bongo katika kundi kubwa:
Ni vitu gani vitatu muhimu tulivyojifunza katika mada za leo?

- Kubadili tabia
- Kupunguza Hatari.
- Hatua za mabadiliko.
- Stadi za kutatua matatizo.
- kuomboleza na Kupotelewa.
- Watoto
- Walezi

Rejea

- Pasztor,E., Blome, W., Cavin, B., Langan, J., Leighton, M., McFadden, E., Olea, M. Petras, D., Polowy, M., Ryan, P.,Sweency-Springwater, J., & Wynne, S. (I 993). *FosterPRIDE/AdoptPRIDE: Preparation and assessment program for foster and adoptive families*. Washington, DC: CWLA.

Siku Ya 6 Kazi Ya Vikundi Kujenga Stadi Kubadili Tabia Na Kutatua Matatizo

- Chagua mwandishi atakaye toa taarifa Kesho asubuhi wakati wa kutoa mrejesho.
- Maswali yanayotokana na mada zilizo fundishwa siku ya leo kuhusu kutumia stadi za kutatua matatizo na stadi za kubadili Tabia.
- Ni mikakati gani ya kufanyia kazi na mtoto, familia na jamii kusaidia kubadili tabia katika kisa mkasa cha kundi lako?
- Fanya kazi katika vikundi vidogo vidogo:
- Gawahya majukumu kama ifuatavyo: Msaidizi ustawi wa jamii,
- Mtoto, au mwana familia/ jirani.
- Fanya igizo dhima kuonyesha msaidizi ustawi , kipindi cha mada inayohusu kusaidia kushughulikia matatizo maalumu au kubadili Tabia.
- Jadilianeni wote kwa pamoja katika kundi kubwa mmejifunza kuhusu mlichojifunza.